

HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

SHULE YA SEKONDARI PROF SARUNGI

S.L.P 02

SHIRATI-RORYA

0784784518/0768625536

MZAZI/MLEZI WA.....

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2021

Nafurahi kukutaarifu kuwa uongozi wa shule pamoja na jumuiya nzima ya shule ya sekondari prof Philemon Sarungi wanakupa pongezi kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga na shule hii kwa mwaka huu wa 2021. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asujbuihi. Mwanao anatakiwa kufika shuleni siku hiyo kwa kuanza masomo rasmi siku hiyo bila kukosa.

SARE YA SHULE (WAVULANA)

Wavulana wanatakiwa kuwa na suruali aina mbili (i) **Rangi nyeusi** (ii) **Rangi ya ugoro**. Suruali zinatakiwa kuwa gredi one. Suruali zote zisishonwe kihuni (modal) miguuni iwe size 18 pia hairuhusiwi kuvaa mtepesho, Nashauri mwanao asinunue suruali sokoni, mnunulie kitambaa na mpe fundi ampime ili aje na suruali inayokubalika. Nguo za kuchukua sokoni mara nyingi hazimtoshi mnunujzi kwa sababu fundi hakumpima.

- ❖ Mashati mawili meupe (yote) mikono mifupi na lazima ziwe za mtumba au Tomato.
- ❖ Viatu vya ngozi vyeusi (soli fupi). Ni marufuku kuvaa viatu aina ya raba shuleni.
- ❖ Soksi nyeusi na mkanda mweusi wa kuvalia suruali.

SARE YA SULE (WASICHANA)

- ❖ Wasichana watakua na sketi za aina mbili. Rangi kama ilivyo kwa wavulana.
- ❖ Sketi zote zinatakiwa kuwa ndefu zinazogusa kisigino (kwa hakika kama sketi ya mwanao haitagusa kisigino uttarudi naye nyumbani ili ikarekebishwe.
- ❖ Masharti (soma hapo juu kwa wavulana).
- ❖ Viatu (kama ilivyo kwa wavulana soksi nyeupe.

KWA WOTE WAVULANA NA WASICHANA

- ❖ Counter book 10 (zote ziwe quire 4). Sitopenda kusumbuana kwa hili suala la counter books.
- ❖ Kalamu zake za kutumia.
- ❖ T-shirt ya blue yenye kola iliyo na michirizi mwiupe.
- ❖ Masweta 2 (i) dark blue (ii) ugoro.
- ❖ Mathematical set na rula ndefu ya plastic.
- ❖ Siku ya kuripoti avae nguo za ugoro suruali/sketi na sweta ugoro.

NB:NI LAZIMA MZAZI AJE NA MWANAFUNZI SIKU YA KURIPOTI.



Richard B Okore
Mkuu wa Shule

